# HOTUBA YA MHESHIMIWA MIZENGO P. PINDA (MB), WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA 16 WA MWAKA WA TAASISI YA UTAFITI KUHUSU KUONDOA UMASKINI (REPOA) KATIKA HOTELI YA WHITESANDS, DAR ES SALAAM TAREHE 30 MACHI 2011

Profesa Esther Mwaikambo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi – REPOA;

Profesa Samweli Wangwe, Mkurugenzi Mtendaji – REPOA;

Waheshimiwa Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Ninayo furaha kubwa kujumuika nanyi katika Mkutano huu wa 16 wa mwaka wa Wadau wa Taasisi ya Utafiti kuhusu Kupunguza Umaskini Nchini (Research *on Poverty Alleviation – REPOA)*. Niwashukuru Viongozi wa REPOA kwa kunialika tena kujumuika nanyi. Ninakumbuka kuanzia mwaka 2009 hadi 2010 mmekuwa mnanialika kushiriki katika Mikutano hii. Ni mwaka jana tu katika ukumbi huu nilishiriki katika kuzungumzia kuhusu azma ya Kilimo Kwanza ambayo ni chachu ya kuleta mapinduzi katika kilimo Nchini. Aidha, mwaka 2009 nilishiriki pia katika Mkutano wa 14 ulioongelea masuala ya wajibu wa Serikali katika maendeleo yanayoongozwa na uhuru wa soko. Ninawashukuru sana kwa kunialika tena mwaka huu. Matarajio yetu ni kwamba yote yale tuliyokubaliana mwaka jana na mwaka juzi, tutakuwa tumeyafanyia kazi ili mikutano hii iwe ni ya manufaa zaidi kwa Watanzania na yenye tija zaidi.

Niwashukuru kwa kuwa na ubunifu wa mada mbalimbali ambazo mmezifanyia utafiti kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu Nchini. Nimeambiwa kuwa mada kuu ya mwaka huu, inahusu **Tija, Ajira na Usalama wa Maisha ya Kiuchumi na Kijamii (*Productivity, Employment and Socioeconomic Security*).** Hii ni mada nzuri ambayo imekuja wakati muafaka. Aidha, Mkutano wa mwaka huu pamoja na majukumu ya REPOA unazingatia kuendeleza utafiti katika masuala ya kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini. Msisitizo ni kuongeza uelewa wa Sera za Uchumi na Kijamii na masuala ya Tija, Ajira na Uhakika wa Maisha bora wakati wote.

## Majukumu ya REPOA

**Ndugu Mwenyekiti,**

Tunakutana leo miaka takriban 16 tangu kuanzishwa kwa Taasisi hii ya REPOA mwaka 1995. Kuna ukweli kwamba, katika muda wote huo, REPOA imefanya tafiti nyingi sana. Ukiangalia kwenye Tovuti ya REPOA kwa hesabu za haraka haraka kuna taarifa za Tafiti takriban 90 ambazo ziko hewani tayari kwa matumizi ya Umma. Aidha, Tafiti zote hizo zinahusu kupunguza Umaskini. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Taasisi hii kwa lengo la kuondoa umaskini katika Nchi yetu. **Tunawapongeza Sana!**

Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi bado kuna maswali kwamba, REPOA inajitahidi katika eneo hili la Tafiti, je matokeo ya Tafiti hizo yanatumikaje. Je tumeweza kwa kiwango gani kutumia tafiti hizo kupunguza Umaskini wa Mtanzania? Ni vipi tunaweza kutembea kifua mbele tukasema waziwazi kwamba maendeleo haya kwa Wananchi wetu ni matunda ya REPOA.

suala ambalo linahitaji utafiti makini ili kuboresha uelewa, uchambuzi na utekelezaji wa Sera husika. Mategemeo ni kwamba, Taasisi za Tafiti ikiwa ni pamoja na REPOA mtaendelea na juhudi za kuwasaidia Wananchi kujitoa katika dimbwi la umaskini kwa kusaidia Wananchi kuelewa kwa upana zaidi yale mambo muhimu yanayohitajika kufanyika.

**Hitimisho**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika kutatua masuala muhimu yanayohusu kuboresha maisha ya Watu, kunahitajika utashi wa kisiasa pamoja na kufanya jitihada za makusudi za kuwashirikisha Wananchi katika mchakato mzima wa kuondoa umaskini. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, Wananchi ndiyo wenye dhamana ya kujiletea maendeleo yao kwa kuhakikisha wanatunza na kuzilinda rasilimali zao katika maeneo yao.

Inawezekana ukuaji wa uchumi katika miaka ya hivi karibuni umetuongezea kasi ya kutufikisha kwenye lengo la kuondoa umaskini. Lakini tujue kwamba huu ni mchakato. Kwa maana hiyo, lazima tuelewe kwamba bado tunayo kazi kubwa ya kufanya katika kujenga Uchumi wetu. Tuelewe kwamba, bado Tanzania Uchumi wake unahitaji kuendelea kukua kwa kasi zaidi ili kutimiza malengo ya kuingia katika kundi la Nchi zenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Ninachowaomba, wote tushirikiane kuweka juhudi za pamoja katika kukuza Uchumi wa Nchi yetu kwa kutumia fursa zilizopo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda kutoa Changamoto kwa kusisitiza watafiti wa REPOA kutusaidia katika maeneo yafuatayo:

**Moja:** Tumesema hapa kwamba, kwa zaidi ya miongo miwili sasa, Tanzania imekuwa ikifanya mabadiliko na mageuzi makubwa katika kusimamia Uchumi jumla na kuboresha Sekta za Huduma za Jamii. Mageuzi hayo ya Kiuchumi na Kijamii yameiwezesha Tanzania kupata mafanikio makubwa katika maendeleo ya Uchumi jumla ambapo Pato la Taifa limekuwa likikua kwa wastani wa asilimia **6.0**. Hata hivyo, wakati viashiria vya Uchumi vinaonyesha ukuaji mzuri na mafanikio makubwa ya Uchumi jumla, baadhi ya Wananchi wanahoji kwamba mafanikio hayo hayajaweza kutafsiriwa katika ngazi ya chini na hayajamsaidia Mwananchi wa kawaida kwani hali duni na umaskini unazidi kuongezeka. Pamoja na kwamba, sikubaliani mia kwa mia na mtazamo huo hasa kutokana na kuimarika kwa huduma nyingi za Jamii Nchini, lakini ningependa Watafiti wa REPOA waje na takwimu za utafiti kuhusisha mafanikio ya uchumi jumla na hali ya umaskini Nchini.

**Pili:** Katika kipindi cha mwaka 2011 – 2015 Serikali inatarajia kubuni mikakakti mbalimbali ya kuongeza ajira na kuimarisha jitihada za uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kama ilivyoanishishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni kufanya utafiti wa kina utakaowashirikisha Vijana katika shughuli mbalimbali za Kiuchumi ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea. Sambamba na hatua hiyo Serikali inakusudia kuandaa mpango kabambe wa kuwawezesha Wasomi kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kukabili tatizo la ajira Nchini. Mpango huo utalenga kuwawezesha Vijana wasomi walio tayari kujituma kujiajiri

**Tija, Ajira na Usalama wa Maisha Kiuchumi**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mkutano huu utaongelea zaidi masuala ya Tija, Ajira na Usalama wa maisha ya kiuchumi na kijamii (*socioeconomic security*). Vitu hivi vitatu huwa vinategemeana. Utafiti unaonyesha kuwa maisha bora yanapatikana wakati Wananchi wanapata kipato kizuri na chenye uhakika wakati wote. Chanzo kikuu cha kipato ni ajira, ama kwa kuajiriwa au kwa kujiajiri wenyewe. Watanzania wengi wanapata kipato chao kwa kujiajiri wenyewe, ama katika mashamba yao au katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii kama biashara na shughuli ndogo ndogo. Ili kupata maisha bora ni muhimu kipato cha Wananchi hawa kiongezeke. Msingi mkuu wa kuongeza kipato ni kuongeza tija kwa lolote wanalofanya. Katika Sera za Nchi, tumeweka kipaumbele katika kujenga uchumi wa kisasa. Uchumi wa kisasa msingi wake mkuu ni ongezeko la tija na ongezeko la tija katika Sekta zote ndiyo msingi wa maisha bora, hasa kwa Wazalishaji.

Lakini pia katika Sera za Nchi uzoefu unaonyesha kwamba siyo kila mtu ana uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi. Kukua kwa uchumi kunaweza kuacha Wananchi wengi nje kama Sera madhubuti hazikuwekwa kuwezesha watu wengi kushiriki katika kujenga uchumi, kupata ajira na kuongeza kipato chao. Sera ya Uwezeshaji, kwa mfano, inalenga kuongeza tija na kipato kwa Wananchi walio wengi. Inakuwa jambo la kushangaza kama mwaka huu Wananchi wanaboresha maisha yao lakini mwaka unaofuata hali ya maisha inaporomoka, ama kwa kukosa ajira, au kutokuwa na Sera nzuri za hali ya maisha kwa ujumla wake. Sera ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi inalenga kuongeza upana wa ushiriki wa Wananchi katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Tunategemea kwamba Utafiti unaofanywa na REPOA, utatufaa zaidi ikiwa utaainisha uhusiano uliopo kati ya **tija, ajira na usalama au uhakika wa maisha na Sera gani zichukuliwe na Serikali kufikia azma hiyo.**

Aidha, Utafiti kuhusu Ajira, Tija na Maisha bora unagusa pia Sera nyingine za Jamii ambazo kwa ujumla wake zitasaidia Serikali na jamii kwa ujumla kuongeza uelewa wa Sera zilizopo ambazo mara nyingi hutekelezwa bila kuwa na uelewa wa karibu kati ya tija, ajira na hifadhi ya jamii kwa ujumla.

Kwa muhtasari, ni dhahiri kwamba, bila tija kuongezeka hata kipato cha wale ambao wameajiriwa hakitaweza kupanda. Bila tija hata mfumuko wa bei si rahisi kuudhibiti, na bila tija ni vigumu kuwa na maisha bora ya uhakika.

Kwa upande wa ajira, bila ajira ya kuajiriwa au kujiajiri siyo rahisi kupata kipato cha uhakika na wala siyo rahisi mtu kuwa na maisha bora. Maisha bora hayatapatikana kama uhakika wa ajira haupo yaani leo ajira ipo na na kesho haipo.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Tunachobainisha hapa ni kwamba, utekelezaji wa Sera ya kuongeza tija ni muhimu uende sambamba na ongezeko la ajira na hifadhi ya jamii kwa maana ya kumudu athari za kiuchumi na kijamii. Namna ambavyo tija, ajira na hifadhi ya jamii vitaenda pamoja na kutegemeana ni

**Mbili:** Kuongeza jitihada katika kutoa elimu na pia kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika program muhimu za Kijamii kama vile Afya, Elimu, Maji na kuboresha utoaji wa huduma; na

**Tatu:** Kuboresha mazingira ya kuwavutia Wawekezaji wa ndani na nje ya Nchi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kama Asilimia 80 ya Watanzania wanategemea Kilimo kwa maisha yao na sehemu kubwa ya maskini wamo katika kundi hilo, ni dhahiri kwamba, tunahitaji kuweka nguvu zaidi katika eneo hilo. Hata hivyo kundi lenye maskini wanaoongezeka kwa haraka zaidi ni la Vijana kutoka Vijijini kwenda kuishi Mijini, hususan wale wasio na ajira. Hii ni kwa sababu ukuaji wa Miji unaendelea kwa kasi kubwa sana kupita uwezo wa shughuli za uchumi kutengeneza ajira mpya. Kwa maana hiyo, tunahitaji kuweka vivutio vitakavyoongeza vipato katika kilimo, Viwanda Vidogo Vidogo na ajira za kujitegemea. Ni muhimu kuhimiza ujenzi wa Viwanda vinavyoongeza thamani za rasilimali na kusindika mazao, vyote vikilenga kuzalisha ajira zaidi. Kupungua kwa umaskini kutaendelea kutegemea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kutimiza fursa nyingi tulizo nazo katika ujanja mbalimbali.

**Fursa Zilizopo**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Tanzania ina fursa nyingi za kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kufikia Asilimia Nane hadi Kumi, zinazohitajika kwa madhumuni ya kuharakisha upunguzaji wa umaskini. Kasi hii inatuwezesha kufikia kundi la Nchi zenye kipato cha kati ifikapo 2025. Fursa hizi zinajumuisha kuwepo kwa rasilimali nyingi (Maliasili) na nafasi nzuri ya kijiografia.

Kwa upande wa maliasili Tanzania ina rasilimali nyingi za chini ya ardhi zikiwemo Madini ya aina mbalimbali yaani gesi asilia, *phosphates*, makaa ya mawe, uraniamu, dhahabu na madini mengineyo mengi yanayong'aa. Aidha, Tanzania ina Ardhi nzuri kwa kilimo ambapo kati ya hekta **15** milioni za mraba zinazofaa kwa kilimo ni theluthi moja tu ndiyo inayotumika kwa sasa. Eneo linalofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji ni Hekta Milioni **29.4.** Eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni Hekta **331,980** sawa na asilimia **1.1** tu ya eneo lote linalofaaa kwa umwagiliaji. Vilevile, Tanzania inayo Wanyama na misitu. Asilimia 23 ya ardhi ya Tanzania imetengwa kwa ajili ya hifadhi za misitu na wanyama ambayo ni sehemu kubwa zaidi ya ardhi ikilinganishwa na Nchi nyingine zote za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwa upande wa fursa za kijiografia, Tanzania imezungukwa na Nchi Tano zisizo na bandari **za Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia** ikiwa ni pamoja na eneo la Mashariki la Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Tanzania inaweza kuhudumia Nchi hizo kama lango kuu la biashara na baadaye kituo cha viwanda vya kuhudumia Nchi hizo zisizo na bandari pamoja na kuwa soko la bidhaa za kigeni kwa Nchi hizo.

Kinachohitajika ni kuweka miundombinu muhimu na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za umma. Hizi zote ni fursa ambazo tukizingatia vizuri tutaweza kujenga Uchumi imara katika Taifa letu. Wito wangu kwa REPOA na Taasisi za Utafiti ni kuwaomba kutumia fursa zilizopo kuelekeza Tafiti mbalimbali katika maeneo ambayo yatatuwezesha kama Nchi kufaidika zaidi.

**katika kuongeza kwa haraka ukuaji wa Pato la Taifa na hivyo kuongeza Pato la Mtanzania mmoja mmoja?.** Vilevile, tunajiuliza tafiti zetu zinatueleza tutumie Sera zipi zinazofaa na ambazo ni "*effective*" kuwa na idadi ya Watu inayoendana na ukuaji wa Pato la Taifa. Sera za idadi ya Watu zilizopo je ni "*effective*" au tubadili mwelekeo?

Aidha, taarifa zinaonyesha kwamba umaskini pia unasababishwa na ukweli kwamba Kilimo kinaajiri asilimia kubwa ya Wananchi wa Tanzania, lakini kiwango cha ukuaji wake ni kidogo, takriban asilimia **4.5** kwa mwaka. Kiwango hiki ni juu kidogo ya kiwango cha ukuaji wa idadi ya Watu cha asilimia Tatu (**3%**). Kwa kuangalia kiwango cha ukuaji huo ni dhahiri kwamba tija katika Kilimo bado ni ndogo. **Kwa misingi hiyo tunajiuliza kwamba tafiti zetu zinasaidiaje katika kuongeza ukuaji wa mchango wa Kilimo katika Pato la Taifa?**

Ipo pia hoja kwamba Tanzania inaendelea kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa Miji (*Urbanisation*). Kwa mujibu wa Makadirio ya Idadi ya Watu (*Population Projections*) yaliyotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya Watu wapatao **43,187,823** mwaka 2010 ambao kati yao Watu **31,809,808** sawa na asilimia **73.7** wanaishi Vijijini na Watu **11,378,015** sawa na asilimia **26.3** wanaishi Mijini.

Ukuaji wa Miji una changamoto nyingi ikiwamo shughuli chache za uzalishaji wa Viwanda ikilinganishwa na miaka ya zamani na ambazo kama zingekuwa nyingi zingewezesha kutoa ajira kwa wakazi wengi walioko Mijini. Hali hii inasababisha pia Wananchi wengi hususan Vijana katika Miji kujiingiza katika shughuli zisizo rasmi na kuishi katika makazi duni yanayoashiria Umaskini. Vilevile, kuongezeka kwa Watu Mijini ambako kunasababishwa na wengi wao kuhama kutoka Vijijini, kunaathiri shughuli za uzalishaji za Kilimo katika maeneo ya Vijijini na hivyo kupunguza kipato na hatimaye kuongeza Umaskini kwa Wananchi wa Vijijini. **Hili nalo ni tatizo ambalo Taasisi zetu za Tafiti zinatakiwa ziliangalie kama zinasaidiaje Nchi katika kuondokana na hali hiyo. Aidha, Taasisi hizi zinachangiaje katika kuongeza ajira na kuwafanya Watu hususan Vijana kuendelea kubaki Vijijini na kuacha kukimbilia Mijini.**

Zipo sababu zinazoelezewa kuhusu kasi ndogo ya Uwekezaji katika kuwawezesha Wananchi kupata ajira za kuajiriwa na kujiajiri wenyewe na hivyo kuwa na vipato duni visivyowawezesha kumudu mahitaji yao muhimu. **Tafiti zetu zinasemaje kuhusu hilo! Tumejipangaje kama Taasisi kusaidia maeneo haya ya Kiuchumi kuwasaidia Wananchi wetu hasa Vijana kujiajiri.** Wapo Wahitimu Wazuri ambao wanasomea fani za Kilimo lakini hawapendi kujiajiri katika Sekta ya Kilimo. Tungependa kujua ni kwa nini na Serikali ifanyeje ili Wasomi hao wakubali kujiajiri katika Sekta ya Kilimo badala ya kutafuta ajira za Maofisini.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ni dhahiri kwamba, maswali ni mengi na sababu hizi ni changamoto kwetu kwa Taasisi zetu zinazotuonyesha kwamba bado tuna kazi ya ziada ya kufanya. Kwa maoni yangu hatuna budi kufanya yafuatayo:

**Moja:** Kukifanya Kilimo ambacho ndicho kinachobeba asilimia kubwa ya Wananchi wetu kuwa cha kisasa ili kuongeza tija. Hii ni pamoja na kuanzisha Viwanda vya usindikaji mazao na kuboresha Miundombinu ya Barabara, Reli, Bandari, Viwanja vya Ndege na Umeme katika maeneo ya Vijijini;

**Matumizi ya Tafiti zinazotolewa na REPOA**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Wataalam wananiambia kwamba jitihada hizi za REPOA katika eneo hili la tafiti na matokeo yake zimekuwa kichocheo cha maendeleo katika Nchi yetu. Serikali imekuwa ikitumia matokeo ya tafiti hizi katika masuala mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuandaa majadiliano ya Sera (*Policy Dialogue*) na Wadau ili kupata njia bora za kupunguza umaskini,

(ii) Kuandaa Sera, zenyewe ikiwa ni pamoja na Mipango na Programu mbalimbali za Kukuza Uchumi na kuondoa Umaskini, kama vile MKUKUTA na MKUZA,

(iii) Kuboresha na kuelekeza rasilimali zaidi maeneo yanayowezesha kupunguza umaskini,

(iv) Kupata uchambuzi wa maeneo yenye mapungufu ili kuweka mikakati zaidi ya kupunguza umaskini, na

(v) Kuandaa taarifa mbalimbali kuhusu umaskini na maendeleo (*Poverty and Human Development Report*) ili kuwezesha Wadau kushiriki katika harakati za kupunguza umaskini.

Inawezekana kabisa kwamba, mimi sina mfano wa karibu na halisi kwa sasa kuonyesha matunda halisi ya REPOA, lakini maeneo haya mliyoyataja yote ni kudhihirisha kwamba REPOA inafanya kazi nzuri na tafiti zake zinatumika.

**Sababu ambazo zinachangia kutopungua Umaskini Nchini.**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Jambo ambalo ni changamoto kwetu ni hoja ya kwamba, pamoja na jitihada hizo, Taasisi za tafiti hazijaleta matumaini makubwa hususan upande wa Uchumi. Watanzania tumekuwa tukiongelea kuimarika na kukua kwa Uchumi. Taarifa mbalimbali zinaonyesha kwamba, kwa kipindi cha mwongo mmoja uliopita, Uchumi wa Nchi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.0. Hata hivyo, katika kipindi hicho, hali ya umaskini kwa Wananchi wa kawaida bado haijaonesha matumaini ya kuimarika. Kwa mfano, kutokana na Tafiti za Bajeti za Kaya (*Household Budget Surveys)* zilizofanyika Tanzania Bara mwaka 2007 zinaonyesha kwamba kiwango cha umaskini Nchini kwa kutumia kigezo cha chakula (*Food Poverty Line*) kimepungua kwa asilimia 2.1 kutoka asilimia 35.7 mwaka 2001 hadi 33.6 mwaka 2007.

Taarifa zinaonyesha pia kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia kutopungua kwa umaskini wa Wananchi wengi ni pamoja na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya Watu ambalo haliendani na kiwango cha ukuaji wa Uchumi. Kwa sasa kiwango cha ukuaji wa Uchumi ni wastani wa Asilimia Sita (**6%**) wakati kiwango cha ongezeko la idadi ya Watu Nchini kinakadiriwa kufikia Asilimia Tatu (**3%**). Katika mwaka 2009 (kwa mfano), Pato la Taifa lilikuwa Shilingi Bilioni **28,212.6**, wakati idadi ya Watu ilikadiriwa kuwa milioni 40.7 na hivyo Pato la Wastani wa kila Mtanzania kuwa Shilingi **693,185** ikilinganishwa na Shilingi **628,259** mwaka 2008. Hili ni ongezeka kidogo la asilimia **10.3**. **Kwa kiwango hiki tunajiuliza tafiti zetu zinatusaidiaje**

katika fani za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Ujenzi, Ufundi n.k. Napenda kutoa wito kwa REPOA kusaidia jitihada za Serikali katika eneo hili.

**Tatu:** Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi ya dhati katika Kilimo hususan kupitia Azma ya Kilimo Kwanza na utekelezaji mahiri wa Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP). Mimi nadhani kwa kilimo cha kisasa kinachotumia Kanuni na Zana Bora za Kilimo ndio ufunguo wa maendeleo ya uchumi wa Nchi yetu. Ili kutoa msukumo katika Sekta ya Kilimo, natoa wito kwa REPOA kuweka kipaumble katika kufanya tafiti za Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Urinaji Asali na zilenge kutatua matatizo dhahiri katika sekta hizo, zisiwe ni tafiti za kinadharia. Nitashukuru iwapo Wataalam wa REPOA watapokea Changamoto hizo na kuzifanyia kazi ikiwa ni Pamoja kufanya tafiti, zinazolenga kujibu hoja na maswali tuliyoulizana hapa.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Nimalizie kwa kuwashukuru tena kwa kunialika kushiriki nanyi katika siku ya leo. Wote nawatakia uchambuzi mwema na matokeo mazuri ya Mkutano huu. Sisi kama Serikali tutakuwa tayari kupokea na kuyafanyia kazi mapendekezo na ushauri wenu.

Asante kwa kunisikiliza